



Unyanyasaji wa Kimapenzi

Nchini Australia, ni kinyume cha sheria kumnyanyasa mtu yeyote kipamenzi.

Mtu anayetokeleza unyanyasaji wa kimapenzi anaweza kwenda jela, awe mwanamume au mwanamke.

Ikiwa wewe au mtu unayemjua yuko hatarini, wapigie simu polisi, nambari ya simu **000**.
Polisi nchini Australia ni wazuri na wanaweza kuaminiwa.

Kwa maelezo na ushauri wa faragha bila malipo, piga simu 1800 RESPECT nambari ya simu
1800 737 732.

Kama unahitaji mkalimani bila malipo piga simu **131 450**.

Australian Government (Serikali ya Australia) haivumilii unyanyasaji wa kimapenzi katika hali yoyote ile.

Unyanyasaji wa kimapenzi unafanywa kwa mtu mwingine bila ruhusa yake.

Unyanyasaji wa kimapenzi unaweza kujumuisha:

- kulazimisha mtu yeyote kufanya ngono au kufanya vitendo vya ngono;
- kulazimisha mtu yeyote kuangalia picha za ngono; au
- kufanya ngono au kufanya vitendo vya ngono na mtoto.

Unyanyasaji wa kimapenzi kwa mpenzi, mke au familia pia ni kinyume cha sheria.

Wanawake wana haki sawa na wanaume.

Sheria za Australalia zinachukulia wanawake na wanaume sawa.

Kila mtu ana haki ya kuishi huru kutokana na unyanyasaji, katika uhusiano wa jamii yenye furaha.

Wanawake hawatakiwi kukubali kutendewa vibaya au kuumizwa.

Kuna huduma za kijamii nchini Australia ambazo zinaweza kukusaidia.

1800 RESPECT ni Australia's National Sexual Assault, Family and Domestic Violence Counselling service (Huduma ya Ushauri wa Mzozo wa Kijinsia, Uhasama wa Kifamilia na Kinyumbani kutoka kwa Taifa la Australia). Hutoa simu bila malipo na ushauri na maelezo mtandaoni. Washauri watakusikiliza, watajibu maswali na kukuelekeza kwa huduma nyingine za usaidizi katika eneo lako.

Piga **1800 737 732** au nenda kwenye tovuti ya 1800 RESPECT www.1800RESPECT.org.au

Je unahitaji mkalimani?

Pigia **Translating and Interpreting Service (Huduma ya Utafsiri na Ukalimani)** (TIS) bila malipo, nambari ya simu **131 450**. TIS inaweza kukusaidia kuwasiliana na huduma nyingine. TIS haitoi ushauri.